# Danieli

## *Mafunzo ya Danieli huko Babeli*

1 Katika mwaka wa tatu wa utawala wa Yehoy-
akimu mfalme wa Yuda, Nebukadneza mfalme
wa Babeli alikuja akazingira Yerusalemu.
2 Bwana akamtia Yehoyakimu mfalme wa Yuda
mkononi mwa Nebukadneza, pamoja na baadhi
ya vyombo kutoka Hekalu la Mungu. Nebukad-
neza akavichukua hadi kwenye hekalu la mungu
wake huko Shinari*, naye akaviweka nyumbani
ya hazina ya mungu wake.
3 Kisha mfalme akamwagiza Ashpenazi, mkuu
wa maafisa wa mfalme, kumletea baadhi ya
Waisraeli kutoka jamaa ya mfalme na kutoka
jamaa kuu:
4 vijana wa kiume wasio na dosari mwilini,
wenye sura nzuri, wanaoonesha kipaji katika
kila aina ya elimu, wenye ufahamu mzuri,
wepesi kuelewa, na waliofuzu kuhudumu katika
jumba la kifalme. Alikuwa awafundishe lugha na
maandiko ya Wakaldayo.
5 Mfalme akawaagizia kiasi cha chakula na
divai ya kila siku kutoka meza ya mfalme. Wa-
likuwa wafundishwe kwa miaka mitatu, na hati-
maye waingie kwenye utumishi wa mfalme.
6 Baadhi ya hawa vijana walitoka Yuda:
Danieli, Hanania, Mishaeli na Azaria.

---

* **1:2** yaani *Babeli*

7 Mkuu wa maafisa akawapa majina mapya: Danieli akamwita jina Belteshaza, Hanania akamwita jina Shadraki, Mishaeli akamwita jina Meshaki, na Azaria akamwita jina Abednego.

8 Lakini Danieli alikusudia kuwa hatajinajisi kwa chakula cha mfalme na divai, naye akamwomba mkuu wa maafisa ruhusa ili asijinajisi kwa njia hii.
9 Basi Mungu alikuwa amemfanya huyo mkuu wa maafisa kuonesha upendeleo na huruma kwa Danieli.
10 Lakini huyo mkuu wa maafisa akamwambia Danieli, "Ninamwogopa bwana wangu mfalme, aliyeagizia chakula na kinywaji chenu. Kwa nini aone nyuso zenu zikiwa mbaya kuliko za vijana wengine wa rika lenu? Mfalme atakata kichwa changu kwa sababu yenu."

11 Ndipo Danieli akamwambia mlinzi aliyeteuliwa na huyo mkuu wa maafisa kuwasimamia Danieli, Hanania, Mishaeli na Azaria,
12 "Tafadhali wajaribu watumishi wako kwa siku kumi. Usitupe chochote ila nafaka na mboga za majani† tule, na maji ya kunywa.
13 Baadaye ulinganishe sura zetu na vijana wanaokula chakula cha mfalme, ukawatendee watumishi wako kulingana na unachoona."
14 Basi akakubali jambo hili, akawajaribu kwa siku kumi.

---

† **1:12** yaani *zeroimu* kwa Kiebrania; ina maana ya aina za ngano na shayiri, na jamii ya kunde kama maharagwe, dengu, choroko, na zingine

15 Mwisho wa zile siku kumi, walionekana
kuwa na afya na kunawiri kuliko yeyote kati ya
vijana waliokula chakula cha mfalme.
16 Hivyo mlinzi wao akaondoa chakula chao
na divai yao waliopangiwa kula na kunywa,
akawapa nafaka na mboga za majani badala
yake.
17 Mungu akawapa hawa vijana wanne maar-
ifa na ufahamu wa kila aina ya maandiko na
elimu. Naye Danieli aliweza kufahamu maono na
aina zote za ndoto.
18 Mwisho wa muda uliowekwa na mfalme ili
kuwaingiza kwake, mkuu wa maafisa akawaleta
mbele ya Mfalme Nebukadneza.
19 Mfalme akazungumza nao, akaona hakuna
aliyelingana na Danieli, Hanania, Mishaeli na
Azaria. Hivyo wakaingia katika utumishi wa
mfalme.
20 Katika kila jambo la hekima na ufahamu
kuhusu kile mfalme alichowauliza, aliwapata
kuwa bora mara kumi zaidi ya waganga na
wasihiri wote katika ufalme wake wote.
21 Naye Danieli akabaki huko hadi mwaka wa
kwanza wa utawala wa Mfalme Koreshi.

# 2

### *Ndoto ya Nebukadneza*

1 Katika mwaka wa pili wa utawala wake,
Nebukadneza aliota ndoto. Mawazo yake yaka-
sumbuka na hakuweza kulala.
2 Hivyo mfalme akawaita waganga, wasihiri,
wachawi, na wanajimu ili wamwambie ndoto

yake aliyokuwa ameota. Walipoingia na kusi-
mama mbele ya mfalme,
3 akawaambia, “Niliota ndoto inayonisumbua,
nami nataka nijue maana yake.”
4 Ndipo wanajimu wakamjibu mfalme kwa
lugha ya Kiaramu*, “Ee mfalme, uishi milele!
Waambie watumishi wako hiyo ndoto, nasi tu-
taifasiri.”
5 Mfalme akawajibu wanajimu, “Nimeamua
hivi kwa uthabiti: Ikiwa hamtaniambia ndoto
yangu ilikuwa ipi na kuifasiri, mtakatwa vipande
vipande, na nyumba zenu zitafanywa kuwa vi-
fusi.
6 Lakini mkiniambia ndoto yangu na kuifasiri,
mtapokea kwangu zawadi, tuzo na heshima
kubwa. Basi niambieni ndoto yangu na mni-
fasirie.”
7 Wakajibu kwa mara nyingine, “Mfalme na
awaambie watumishi wake ndoto yake, nasi tu-
taifasiri.”
8 Ndipo mfalme akajibu, “Nina hakika kuwa
mnajaribu kupata muda zaidi, kwa sababu
mnatambua kuwa nimeamua hivi kwa uthabiti:
9 Ikiwa hamtaniambia ndoto yangu, ipo ad-
habu moja tu kwenu. Mmepanga njama kuni-
ambia habari za kunipotosha na mambo maovu,
mkitumaini kwamba hali itabadilika. Hivyo
basi, niambieni hiyo ndoto, nami nitajua kuwa
mwaweza kunifasiria.”
10 Wanajimu wakamjibu mfalme, “Hakuna mtu
duniani ambaye anaweza kufanya analotaka
mfalme! Vilevile, hakuna mfalme, hata awe

* **2:4** Kutoka hapa hadi Danieli 7:28, mwandishi aliandika na Kiaramu.

mkuu na mwenye uweza namna gani, aliyeuliza
kitu kama hicho kwa mganga, au kwa msihiri,
wala kwa mnajimu yeyote.
11 Anachouliza mfalme ni kigumu mno.
Hakuna yeyote awezaye kumfunulia mfalme
isipokuwa miungu, nao hawaishi miongoni mwa
wanadamu.”
12 Jambo hili lilimkasirisha na kumghadhibisha
mfalme mno, hata kuagiza kuuawa kwa wenye
hekima wote wa Babeli.
13 Hivyo amri ikatolewa ya kuwaua wenye
hekima, nao watu wakatumwa kuwatafuta
Danieli na rafiki zake ili wawaue.
14 Arioko, mkuu wa askari wa walinzi wa
mfalme, alipokuwa ameenda kuwaua wenye
hekima wa Babeli, Danieli akazungumza naye
kwa hekima na busara.
15 Akamuuliza huyo afisa wa mfalme, “Kwa nini
mfalme ametoa amri kali hivyo?” Ndipo Arioko
akamweleza Danieli jambo hilo.
16 Basi Danieli akawaendea mfalme, akam-
womba ampe muda ili aweze kumfasiria ile
ndoto.
17 Ndipo Danieli akarudi nyumbani mwake
na kuwaeleza rafiki zake Hanania, Mishaeli na
Azaria jambo hilo.
18 Aliwasihi waombe rehema kutoka kwa
Mungu wa mbinguni kuhusu siri hii, ili yeye na
rafiki zake wasije wakauawa pamoja na wenye
hekima wengine wa Babeli.
19 Wakati wa usiku, lile fumbo lilifunuliwa kwa
Danieli katika maono. Ndipo Danieli akamhimidi
Mungu wa mbinguni,
20 akasema:

"Lihimidiwe jina la Mungu milele na milele;
hekima na uweza ni vyake.
21 Yeye hubadili nyakati na majira;
huwaweka wafalme na kuwaondoa.
Huwapa hekima wenye hekima,
na maarifa wenye ufahamu.
22 Hufunua siri na mambo yaliyofichika;
anajua yale yaliyo gizani,
nayo nuru hukaa kwake.
23 Ninakushukuru na kukuhimidi, Ee Mungu wa baba zangu:
Umenipa hekima na uwezo;
umenijulisha kile tulichokuomba,
umetujulisha ndoto ya mfalme."

### *Danieli aifasiri ndoto*

24 Ndipo Danieli akamwendea Arioko, ambaye mfalme alikuwa amemteua kuwaua wenye hekima wa Babeli, akamwambia, "Usiwaue wenye hekima wa Babeli. Nipeleke kwa mfalme, nami nitamfasiria ndoto yake."

25 Arioko akampeleka Danieli kwa mfalme mara moja na kumwambia, "Nimempata mtu miongoni mwa watu wa uhamisho kutoka Yuda ambaye anaweza kumwambia mfalme maana ya ndoto yake."

26 Mfalme akamuuliza Danieli (aliyeitwa pia Belteshaza), "Je, unaweza kuniambia nilichoona katika ndoto yangu na kuifasiri?"

27 Danieli akajibu, "Hakuna mwenye hekima, msihiri, mganga au mwaguzi anayeweza kumweleza mfalme siri aliyouliza,

28 lakini yuko Mungu mbinguni afunuaye siri. Amemwonesha Mfalme Nebukadneza kitakachotokea siku zijazo. Ndoto yako na maono yaliyopita mawazoni mwako ulipokuwa umelala kitandani mwako ni haya:

29 “Ee mfalme, ulipokuwa umelala kitandani, yalikujia mawazo kuhusu mambo yatakayotokea baadaye, naye mfunuaji wa siri akakuonesha ni kitu gani kitakachotokea.
30 Kwangu mimi, nimefunuliwa siri hii, si kwa sababu nina hekima kubwa kuliko watu wengine wanaoishi, bali ili wewe, ee mfalme, upate kujua tafsiri, na ili uweze kuelewa kile kilichopita mawazoni mwako.
31 “Ee mfalme, ulitazama, na mbele yako ilisimama sanamu kubwa mno, iliyong’aa kupita kiasi na yenye kutisha kwa mwonekano wake.
32 Kichwa cha sanamu hiyo kilikuwa kimetengenezwa kwa dhahabu safi; kifua chake na mikono yake vilikuwa vya fedha; tumbo lake na mapaja yake vilikuwa vya shaba;
33 miguu yake ilikuwa ya chuma; na nyayo zake zilikuwa chuma na sehemu nyingine udongo uliochomwa.
34 Ulipokuwa unaangalia, jiwe lilikatwa, lakini si kwa mikono ya mwanadamu. Lile jiwe liliipiga ile sanamu kwenye nyayo zake za chuma na udongo, na kuivunja.
35 Ndipo ile chuma, ule udongo, ile shaba, ile fedha na ile dhahabu vikavunjika vipande vipande kwa wakati mmoja, na vikawa kama makapi katika sakafu ya kupuria nafaka wakati wa kiangazi. Upepo ukavipeperusha bila kuacha

hata alama. Lakini lile jiwe lililoipiga ile sanamu
likawa mlima mkubwa mno na kuijaza dunia
yote.

36 “Hii ndio ilikuwa ndoto, nasi sasa tutam-
fasiria mfalme.
37 Ee mfalme, wewe ni mfalme wa wafalme.
Mungu wa mbinguni amekupa wewe utawala,
uweza, nguvu, na utukufu.
38 Mikononi mwako amewaweka wanadamu,
wanyama wa kondeni, na ndege wa angani.
Popote wanapoishi, amekufanya wewe kuwa
mtawala wa hao wote. Wewe ndiwe kile kichwa
cha dhahabu.
39 “Baada yako, ufalme mwingine utainuka,
ulio dhaifu kuliko wako. Baadaye utafuata
ufalme wa tatu, ule wa shaba, nao utaitawala
dunia yote.
40 Hatimaye kutakuwako na ufalme wa nne,
wenye nguvu kama chuma, kwa maana chuma
huvunja na kupondaponda kila kitu; kama vile
chuma ivunjavyo vitu vipande vipande, ndi-
vyo ufalme huo utakavyopondaponda na kuvun-
javunja nyingine zote.
41 Kama ulivyoona nyayo na vidole, sehemu
moja vikiwa vya udongo uliochomwa na sehemu
nyingine vya chuma, kadhalika ufalme huu
utakuwa umegawanyika; hata hivyo, utakuwa
wenye nguvu ya chuma ndani yake kama
ulivyoona chuma kikiwa kimechanganywa na
udongo.
42 Kama vile vidole vyake vya miguu vilikuwa
kwa sehemu chuma na kwa sehemu udongo,
ndivyo ufalme huo kwa sehemu utakuwa na

nguvu na kwa sehemu udhaifu.
43 Kama ulivyoona nyayo na vidole, sehemu
moja vikiwa vya udongo uliochomwa na se-
hemu nyingine vya chuma, kadhalika ufalme
huu utakuwa umegawanyika; wala hawatabaki
wameungana tena, kama vile chuma kisivy-
oweza kuchanganyikana na udongo.
44 “Katika siku za wafalme hao, Mungu wa
mbinguni atauweka ufalme ambao kamwe hau-
taangamizwa, wala hautaachiwa taifa lingine.
Utaziponda zile falme zote na kuzikomesha, bali
wenyewe utadumu milele.
45 Hii ndiyo maana ya maono ya jiwe lililo-
chongwa kutoka mlimani, lakini si kwa mikono
ya mwanadamu, lile jiwe ambalo lilivunja
chuma, shaba, udongo, fedha na dhahabu
vipande vipande.

“Mungu Mkuu amemwonesha mfalme kile ki-
takachotendeka wakati ujao. Ndoto hii ni ya
kweli, na tafsiri yake ni ya kuaminika.”
46 Ndipo Mfalme Nebukadneza akaanguka ki-
fudifudi mbele ya Danieli kumpa heshima, akaa-
giza wamtolee Danieli sadaka na uvumba.
47 Mfalme akamwambia Danieli, “Hakika
Mungu wako ni Mungu wa miungu, na Bwana wa
wafalme, na mfunuaji wa siri zote, kwa maana
umeweza kufunua siri hii.”
48 Ndipo mfalme akamweka Danieli nafasi ya
juu, na kumpa zawadi nyingi tele. Akamfanya
mtawala wa jimbo lote la Babeli, na kumweka
kuwa mkuu wa wenye hekima wote.
49 Zaidi ya hayo, kwa ombi la Danieli, mfalme
akawateua Shadraki, Meshaki na Abednego

kuwa wasimamizi wa jimbo la Babeli, huku Danieli akibaki katika ukumbi wa mfalme.

# 3

## *Sanamu ya dhahabu na tanuru la moto*

1 Mfalme Nebukadneza alitengeneza sanamu ya dhahabu, yenye kimo cha dhiraa sitini*, na upana wa dhiraa sita†, akaisimamisha kwenye tambarare ya Dura katika jimbo la Babeli.

2 Kisha mfalme akaita wakuu, wasimamizi, watawala, washauri, watunza hazina, waamuzi, mahakimu, na maafisa wengine wote wa jimbo kuja kuizindua sanamu ambayo Mfalme Nebukadneza alikuwa ameisimamisha.

3 Basi wakuu, wasimamizi, watawala, washauri, watunza hazina, waamuzi, mahakimu, na maafisa wengine wote wa jimbo wakakusanyika ili kuizindua sanamu ile Mfalme Nebukadneza alikuwa ameisimamisha, nao wakasimama mbele ya hiyo sanamu.

4 Ndipo mpiga mbiu akatangaza kwa sauti kubwa, “Enyi watu wa makabila yote, na mataifa, na wa kila lugha, hili ndilo mnaloamriwa kulifanya:

5 Mara mtakaposikia sauti ya baragumu, filimbi, marimba, zeze, kinubi, zumari, na aina zote za sauti za ala za uimbaji, lazima msujudu na kuabudu sanamu ya dhahabu ambayo Mfalme Nebukadneza ameisimamisha.

---

* **3:1** Dhiraa sitini ni sawa na mita 27. † **3:1** Dhiraa sita ni sawa na mita 2.7.

6 Mtu ambaye hataanguka chini na kuiabudu sanamu hiyo, atatupwa saa hiyo hiyo ndani ya tanuru linalowaka moto.”

7 Kwa hiyo, mara waliposikia sauti ya baragumu, filimbi, marimba, zeze, kinubi, zumari, na aina zote za sauti za ala za uimbaji, watu wa makabila yote, na mataifa, na wa kila lugha wakasujudu na kuiabudu ile sanamu ya dhahabu ambayo Mfalme Nebukadneza alikuwa ameisimamisha.

8 Wakati huo baadhi ya Wakaldayo walijitokeza na kuwashtaki Wayahudi.

9 Wakamwambia Mfalme Nebukadneza, “Ee mfalme, uishi milele!

10 Ee mfalme, umetoa amri kwamba kila mmoja atakayesikia sauti ya baragumu, filimbi, marimba, zeze, kinubi, zumari, na aina zote za sauti za ala za uimbaji, lazima asujudu na kuiabudu ile sanamu ya dhahabu,

11 na kwamba yeyote ambaye hatasujudu na kuiabudu atatupwa saa hiyo hiyo ndani ya tanuru linalowaka moto.

12 Lakini wako baadhi ya Wayahudi ambao umewaweka juu ya mambo ya jimbo la Babeli, yaani Shadraki, Meshaki na Abednego, ambao hawakujali wewe, ee mfalme. Hawaitumikii miungu yako wala kuiabudu ile sanamu ya dhahabu uliyoisimamisha.”

13 Mfalme Nebukadneza, akiwa amekasirika na mwenye ghadhabu kali, akawaita Shadraki, Meshaki na Abednego. Hivyo watu hawa wakaletwa mbele ya mfalme,

14 naye Nebukadneza akawauliza, “Je, ni kweli
kwamba ninyi Shadraki, Meshaki na Abednego
hamuitumikii miungu yangu wala kuiabudu
sanamu ya dhahabu niliyoisimamisha?
15 Basi wakati mtakaposikia sauti ya baragumu,
filimbi, marimba, zeze, kinubi, zumari na aina
zote za ala za uimbaji, kama mtakuwa tayari
kusujudu na kuiabudu hiyo sanamu niliyoiten-
geneza, vyema sana. Lakini kama hamta-
iabudu, mtatupwa saa hiyo hiyo ndani ya tanuru
linalowaka moto. Naye ni mungu yupi ataweza
kuwaokoa ninyi kutoka mkononi mwangu?”
16 Shadraki, Meshaki na Abednego wakamjibu
mfalme, “Ee Nebukadneza, hatuhitaji kujitetea
mbele zako kuhusu jambo hili.
17 Ikiwa tutatupwa ndani ya tanuru linalowaka
moto, Mungu tunayemtumikia anaweza ku-
tuokoa na moto, naye atatuokoa kutoka mkononi
mwako, ee mfalme.
18 Lakini hata ikiwa hatatuokoa, ee mfalme,
tunataka ufahamu kwamba hatutaitumikia mi-
ungu yako wala kuiabudu sanamu ya dhahabu
uliyoisimamisha.”
19 Ndipo Nebukadneza akawa na ghadhabu
kali sana kwa Shadraki, Meshaki na Abednego,
nayo nia yake ikabadilika kwao. Akaagiza tanuru
lichochewe moto mara saba kuliko kawaida yake,
20 na akawaamuru baadhi ya askari wake
wenye nguvu zaidi katika jeshi lake kuwafunga
Shadraki, Meshaki na Abednego, na kuwatupa
ndani ya tanuru lililowaka moto.
21 Hivyo watu hawa walifungwa na kutupwa
ndani ya tanuru hilo wakiwa wamevaa majoho

yao, suruali, vilemba, na nguo zao nyingine.
22 Amri ya mfalme ilikuwa ya haraka sana na
tanuru lilikuwa na moto mkali kiasi kwamba
miali ya moto iliwaua wale askari waliowapeleka
Shadraki, Meshaki na Abednego.
23 Watu hawa watatu walianguka ndani ya
tanuru hilo la moto wakiwa wamefungwa kwa
uthabiti sana.
24 Ndipo Mfalme Nebukadneza akashangaa,
akainuka kwa haraka na kuwauliza washauri
wake, "Je, hawakuwa watu watatu ambao tuliwa-
funga na kuwatupa ndani ya moto?"

Washauri wakajibu, "Hakika, ee mfalme."

25 Mfalme akasema, "Tazama! Naona watu
wanne wakitembeatembea ndani ya moto; hawa-
jafungwa wala kudhurika, naye mtu yule wa nne
anaonekana kama mwana wa miungu."

26 Ndipo Nebukadneza akaukaribia mdomo wa
lile tanuru lililowaka moto na kuita kwa sauti
kuu, "Shadraki, Meshaki na Abednego, watu-
mishi wa Mungu Aliye Juu Sana, tokeni! Njooni
hapa!"

Ndipo Shadraki, Meshaki na Abednego waka-
toka ndani ya moto.
27 Nao maliwali, wasimamizi, watawala na
washauri wa mfalme wakakusanyika kuwazun-
guka. Waliona kwamba moto haukudhuru miili
yao, wala unywele wa vichwa vyao haukuungua,
majoho yao hayakuungua, wala hawakuwa na
harufu ya moto.

28 Ndipo Nebukadneza akasema, "Ahimidiwe
Mungu wa Shadraki, Meshaki na Abednego, am-
baye amemtuma malaika wake na kuwaokoa

watumishi wake. Walimtumaini na kukaidi amri
ya mfalme, nao wakawa tayari kufa kuliko ku-
tumikia au kuabudu mungu mwingine yeyote
isipokuwa Mungu wao.
29 Kwa hiyo ninaamuru kwamba watu wa
taifa lolote au lugha yoyote watakaosema kitu
chochote dhidi ya Mungu wa Shadraki, Me-
shaki na Abednego wakatwe vipande vipande, na
nyumba zao zifanywe kuwa malundo ya kokoto,
kwa maana hakuna mungu mwingine awezaye
kuokoa namna hii.”
30 Kisha mfalme akawapandisha vyeo
Shadraki, Meshaki na Abednego katika jimbo
la Babeli.

# 4

*Ndoto ya Nebukadneza ya mti*

1 Mfalme Nebukadneza,

Kwa watu wa makabila yote, na mataifa, na wa kila lugha wanaoishi duniani kote:

Mafanikio yawe kwenu sana!

2 Ni furaha yangu kuwaambia kuhusu ishara za miujiza na maajabu ambayo Mungu Aliye Juu Sana amenifanyia.

3 Ishara zake ni kuu kama nini!
Na maajabu yake yana nguvu kama nini!
Ufalme wake ni ufalme wa milele;
enzi yake hudumu kizazi hadi kizazi.

4 Mimi, Nebukadneza, nilikuwa nyumbani katika jumba langu la kifalme, nikiishi kwa raha na mafanikio.

5 Niliota ndoto iliyoniogopesha. Nilipokuwa
nimelala kitandani mwangu, njozi na maono
yaliyopita mawazoni mwangu vilinitisha.
6 Hivyo nikaagiza kwamba wenye hekima
wote wa Babeli waletwe mbele yangu kunifasiria
ndoto yangu.
7 Waganga, wasihiri, wanajimu na waaguzi
walipokuja, niliwaambia ndoto yangu, lakini
hawakuweza kunifasiria.
8 Mwishoni, Danieli alikuja mbele yangu,
nikamweleza hiyo ndoto. (Danieli anaitwa Bel-
teshaza, kwa jina la mungu wangu, nayo roho ya
miungu mitakatifu inakaa ndani yake.)
9 Nikasema, “Belteshaza, mkuu wa waganga,
ninajua kuwa roho ya miungu mitakatifu iko
ndani yako, wala hakuna siri iliyo ngumu
kwako. Hii ndiyo ndoto yangu, nifasirie.
10 Haya ndio maono niliyoona nilipokuwa
nimelala kitandani mwangu: Nilitazama, na
mbele yangu ulisimama mti katikati ya nchi.
Ulikuwa mrefu sana.
11 Mti ule ulikua, ukawa mkubwa na wenye
nguvu, nayo ncha yake ikagusa anga; ulionekana
hadi miisho ya dunia.
12 Majani yake yalikuwa ya kupendeza,
matunda yake yalikuwa mengi, na juu yake ku-
likuwa na chakula kwa ajili ya wote. Chini ya
kivuli chake wanyama wa kondeni walipata hi-
fadhi, na ndege wa angani waliishi katika matawi
yake. Kila kiumbe kililishwa kutokana na mti
huo.
13 “Katika maono niliyoyaona nikiwa nime-
lala kitandani mwangu, nilitazama, na mbele

yangu nikaona mlinzi, aliye mtakatifu, akishuka kutoka mbinguni.

14 Akaita kwa sauti kubwa: 'Kateni mti huu,
myafyeke matawi yake; yaondoeni majani yake
na kuyatawanya matunda yake. Wanyama na
wakimbie kutoka chini yake, na ndege waondoke
kutoka matawi yake.

15 Lakini kiacheni kisiki na mizizi yake,
kikiwa kimefungwa kwa chuma na shaba, kibaki
ardhini, kwenye majani ya kondeni.

" 'Mwacheni aloweshwe na umande wa mbinguni, naye aachwe aishi pamoja na wanyama miongoni mwa mimea ya dunia.

16 Akili yake na ibadilishwe kutoka ile ya
mwanadamu, na apewe akili ya mnyama, hadi
nyakati saba zipite juu yake.

17 " 'Uamuzi huu umetangazwa na wajumbe;
watakatifu, wametangaza hukumu ili walio hai wajue kuwa Aliye Juu Sana ndiye anayetawala katika falme zote za dunia, naye humpa amtakaye, na kumtawaza juu yake hata yeye aliye mnyonge sana miongoni mwa wanadamu.'

18 "Hii ndiyo ndoto niliyoipata mimi, Mfalme
Nebukadneza. Sasa Belteshaza, niambie maana yake, kwa maana hakuna hata mmoja wa wenye hekima katika ufalme wangu anayeweza kunifasiria. Bali wewe unaweza, kwa sababu roho ya miungu mitakatifu iko ndani yako."

### *Danieli anaifasiri ndoto*

19 Ndipo Danieli (aliyeitwa pia Belteshaza)
alipofadhaika sana kwa muda, nayo mawazo

yake yakamtia hofu. Basi mfalme akasema,
“Belteshaza, usiruhusu ndoto wala maana yake
kukutia hofu.”

Belteshaza akajibu, “Bwana wangu, laiti
ndoto hii ingewahusu adui zako, na maana
yake iwahusu watesi wako!

20 Mti uliouona, uliokua ukawa mkubwa na
wenye nguvu, nayo ncha yake ikagusa anga na
kuonekana duniani kote,

21 ukiwa na majani ya kupendeza na
matunda mengi, ukitoa chakula kwa wote, na
ukiwapa hifadhi wanyama wa kondeni, na kuwa
mahali pa viota katika matawi yake kwa ajili ya
ndege wa angani:

22 Ee mfalme, wewe ndiwe ule mti!
Umekuwa mkubwa na mwenye nguvu; nao
ukuu wako umekua hadi kufika juu angani, nayo
mamlaka yako yameenea hadi miisho ya dunia.

23 “Ee mfalme, wewe ulimwona mlinzi,
aliye mtakatifu, akishuka kutoka mbinguni,
akasema, ‘Ukateni mti na kuuangamiza,
lakini kiacheni kisiki kikiwa kimefungwa
kwa chuma na shaba, kwenye majani
ya kondeni, wakati mizizi yake inabaki
ardhini. Mwacheni aloweshwe na umande
wa mbinguni, mwacheni aishi kama wanyama
pori hadi nyakati saba zipite juu yake.’

24 “Ee mfalme, hii ndiyo tafsiri, na hii ni amri
ya Aliye Juu Sana aliyoitoa dhidi ya bwana
wangu mfalme:

25 Wewe utafukuzwa mbali na wanadamu,
nawe utaishi pamoja na wanyama pori; utakula
nyasi kama ng’ombe, na kuloana kwa umande

wa mbinguni. Nyakati saba zitapita hadi utakapokubali kuwa Yeye Aliye Juu Sana ndiye anayetawala katika falme zote za wanadamu, naye humtawaza yeyote amtakaye.

26 Amri ya kuacha kisiki pamoja na mizizi yake inamaanisha kwamba ufalme wako utarejeshwa kwako utakapokubali kwamba Mbingu ndizo hutawala.

27 Kwa hiyo, ee mfalme, uwe radhi kupokea ushauri wangu: Acha dhambi zako kwa kutenda yaliyo haki, ukaache uovu wako na uwe na huruma kwa waliodhulumiwa. Hivyo itawezekana baada ya hayo, mafanikio yako yataendelea."

## *Ndoto inatimia*

28 Haya yote yalimpata Mfalme Nebukadneza.

29 Miezi kumi na mbili baadaye, mfalme alipokuwa akitembea juu ya paa la jumba la kifalme la Babeli,

30 alisema, "Je, huu si Babeli mji mkuu nilioujenga uwe makao ya kifalme, kwa uwezo wangu mkubwa, na kwa ajili ya utukufu wa enzi yangu?"

31 Maneno hayo yalikuwa bado katika midomo yake wakati sauti ilipokuja kutoka mbinguni, ikisema, "Mfalme Nebukadneza, hiki ndicho kilichoamriwa kwa ajili yako: Mamlaka yako ya ufalme yameondolewa kwako.

32 Utafukuzwa mbali na wanadamu, ukaishi pamoja na wanyama pori, na utakula nyasi kama ng'ombe. Nyakati saba zitapita juu yako, hadi utakapokubali kuwa Yeye Aliye Juu Sana ndiye

anayetawala katika falme zote za wanadamu,
naye humtawaza yeyote amtakaye.”
33 Papo hapo yale yaliyokuwa yamesemwa
kuhusu Nebukadneza yakatimia. Alifukuzwa
mbali na wanadamu, akala nyasi kama
ng’ombe. Mwili wake uliloweshwa kwa
umande wa mbinguni, hadi nywele zake
zikakua kama manyoya ya tai, nazo kucha
zake kama makucha ya ndege.

34 Mwisho wa wakati huo, mimi Nebukad-
neza niliinua macho yangu kuelekea mbin-
guni, nazo fahamu zangu zikanirudia. Ndipo
nikamsifu Yeye Aliye Juu Sana, nikamheshimu
na kumhimidi yeye aishiye milele.

Utawala wake ni utawala wa milele;
ufalme wake hudumu kizazi hadi kizazi.
35 Mataifa yote ya dunia
yanahesabiwa kuwa si kitu.
Hufanya kama atakavyo
kwa majeshi ya mbinguni,
na kwa mataifa ya dunia.
Hakuna anayeweza kuuzuia mkono wake
au kumwambia, “Umefanya nini wewe?”

36 Wakati huo huo fahamu zangu ziliponiru-
dia, nikarudishiwa heshima yangu na fahari
yangu kwa ajili ya utukufu wa ufalme wangu.
Washauri wangu na wakuu wangu walikuja
kunitafuta, nami nikarudishwa kwenye kiti
changu cha ufalme, hata nikawa mkuu kuliko
mwanzoni.
37 Basi mimi, Nebukadneza, humhimidi, na
humtukuza na kumsifu Mfalme wa mbinguni,

kwa sababu kila kitu anachofanya ni haki, na njia zake zote ni adili. Nao wanaoenda kwa kiburi anaweza kuwashusha.

# 5

*Maandishi ukutani*

1 Mfalme Belshaza aliandaa karamu kubwa kwa ajili ya wakuu wake elfu moja, na akanywa mvinyo pamoja nao.

2 Belshaza alipokuwa akinywa divai, aliamuru vile vikombe vya dhahabu na fedha ambavyo Nebukadneza baba yake alikuwa amevichukua kutoka hekalu huko Yerusalemu viletwe, ili mfalme na wakuu wake, pamoja na wake zake na masuria wake wapate kuvinywea.

3 Kwa hiyo wakavileta vile vikombe vya dhahabu ambavyo vilikuwa vimechukuliwa kutoka hekalu la Mungu huko Yerusalemu, naye mfalme na wakuu wake, pamoja na wake zake na masuria wake wakavinywea.

4 Walipokuwa wakinywa divai, wakaisifu miungu ya dhahabu na fedha, ya shaba, chuma, miti na mawe.

5 Ghafula vidole vya mkono wa mwanadamu vilitokea na kuandika juu ya chokaa ya ukuta, karibu na kinara cha taa ndani ya jumba la mfalme. Mfalme akatazama kitanga kilivyokuwa kikiandika.

6 Uso wa mfalme ukageuka rangi, naye akaogopa sana, kiasi kwamba magoti yake yaligongana na miguu yake ikalegea.

7 Mfalme akawaita wasihiri, wanajimu na waaguzi waletwe, naye akawaambia hao wenye hekima wa Babeli, “Yeyote asomaye maandishi

haya na kuniambia maana yake atavikwa nguo
za zambarau, na kuvikwa mkufu wa dhahabu
shingoni mwake, naye atafanywa mtawala wa
cheo cha tatu katika ufalme."
8 Ndipo wenye hekima wote wa mfalme
wakaingia, lakini hawakuweza kusoma yale
maandishi wala kumwambia mfalme maana
yake.
9 Basi Mfalme Belshaza akazidi kujawa na hofu,
na uso wake ukageuka rangi zaidi. Wakuu wake
wakapigwa na bumbuazi.
10 Malkia* aliposikia sauti za mfalme na
wakuu wake, alikuja katika ukumbi wa karamu.
Akasema, "Ee mfalme, uishi milele! Usishtuke!
Usibadilike rangi hivyo!
11 Yuko mtu katika ufalme wako mwenye roho
ya miungu mitakatifu ndani yake. Wakati wa
baba yako, mtu huyo alionekana kuwa na ufa-
hamu, akili na hekima kama ile ya miungu.
Mfalme Nebukadneza baba yako, naam, mfalme
baba yako, alimweka kuwa mkuu wa waganga,
wasihiri, wanajimu na waaguzi.
12 Mtu huyu Danieli, ambaye mfalme alimwita
Belteshaza, alionekana kuwa na akili nyepesi,
maarifa na ufahamu, pia uwezo wa kufasiri
ndoto, kueleza mafumbo, na kutatua matatizo
magumu. Mwite Danieli, naye atakuambia
maana ya haya maandishi."
13 Hivyo Danieli akaletwa mbele ya mfalme,
naye mfalme akamuuliza, "Je, wewe ndiwe
Danieli, mmoja wa watu wa uhamisho walio-
letwa na mfalme baba yangu kutoka Yuda?

* **5:10** au *mama malkia* au *mamaye mfalme*

14 Nimesikia kwamba roho ya miungu iko
ndani yako, na kwamba una ufahamu, akili na
hekima ya pekee.
15 Watu wenye hekima na wasihiri waliletwa
mbele yangu ili kusoma maandishi haya na ku-
niambia maana yake, lakini hawakuweza kuni-
fafanulia.
16 Basi nimesikia kwamba unaweza kutoa
tafsiri na kutatua matatizo magumu. Ikiwa
unaweza kusoma maandishi haya na kuniambia
maana yake, utavikwa nguo za zambarau na
mkufu wa dhahabu shingoni mwako, nawe
utafanywa mtawala wa tatu katika ufalme."
17 Ndipo Danieli akamjibu mfalme, "Unaweza
kubaki na zawadi zako mwenyewe na kumpa
mtu mwingine thawabu zako. Hata hivyo, ni-
tasoma maandishi kwa mfalme na kumwambia
maana yake.
18 "Ee mfalme, Mungu Aliye Juu Sana alimpa
baba yako Nebukadneza utawala, ukuu, utukufu
na fahari.
19 Kwa sababu ya ukuu aliompa baba yako,
watu wa makabila yote, na mataifa, na wa
kila lugha walimhofu na kumwogopa. Wale
ambao mfalme alitaka kuwaua, aliwaua; wale
aliotaka kuwaacha hai, aliwaacha hai; wale alio-
taka kuwapandisha cheo, aliwapandisha; alio-
taka kuwashusha, aliwashusha.
20 Lakini moyo wake ulipokuwa na majivuno
na kuwa mgumu kwa kiburi, aliondolewa kutoka
kwa kiti chake cha ufalme na kuvuliwa utukufu
wake.
21 Akafukuzwa mbali na wanadamu na ku-
pewa akili ya mnyama, akaishi pamoja na punda-

mwitu; akala majani kama ng'ombe, nao mwili
wake ukaloweshwa kwa umande wa mbingu,
hadi alipotambua kwamba Mungu Aliye Juu Sana
ndiye mtawala katika falme zote za wanadamu,
na kwamba humtawaza juu yao yeyote am-
takaye.
22 "Lakini wewe mwanawe, ee Belshaza, huku-
jinyenyekeza, ingawa ulifahamu haya yote.
23 Badala yake, umejiinua dhidi ya Bwana
wa mbingu. Uliletewa vikombe vya Hekalu
lake, nawe na wakuu wako, pamoja na wake
zako na masuria wako mlivitumia kwa kuny-
wea divai. Uliisifu miungu ya fedha na dha-
habu, ya shaba, chuma, miti na mawe, mi-
ungu ambayo haiwezi kuona, au kusikia wala
kufahamu. Lakini hukumheshimu Mungu am-
baye anaushikilia uhai wako na njia zako zote
mkononi mwake.
24 Kwa hiyo ameutuma mkono ule ulioandika
maneno.
25 "Haya ndio maneno yaliyoandikwa:

MENE, MENE,
TEKELI, NA PERESI

26 "Hii ndiyo maana ya maneno haya:
"*Mene*: Mungu amezihesabu siku za utawala
wako na kuukomesha.
27 "*Tekeli*: Wewe umepimwa katika mizani na
kuonekana umepungua.
28 "*Peresi*: Ufalme wako umegawanywa na
kupewa Wamedi na Waajemi."
29 Kwa amri ya Belshaza, Danieli akavikwa
nguo za zambarau na mkufu wa dhahabu shin-
goni, tena akatangazwa kuwa mtawala wa tatu
katika ufalme.

30 Usiku ule ule, Belshaza mfalme wa Wakal-
dayo akauawa,
31 naye Dario Mmedi akanyakua ufalme akiwa
na miaka sitini na mbili.

# 6

*Danieli katika tundu la simba*

1 Ilimpendeza Dario kuteua wakuu mia moja
na ishirini kutawala katika ufalme wake wote,
2 pamoja na wasimamizi watatu juu yao,
Danieli akiwa mmoja wao. Wakuu walitoa
hesabu kwa wasimamizi hao ili mfalme asipate
hasara.
3 Basi Danieli alijidhihirisha miongoni mwa
wasimamizi na wakuu kwa sifa zake za kipekee,
hata mfalme akapanga kumweka juu ya ufalme
wote.
4 Walipofahamu hilo, wasimamizi na wakuu
wakajaribu kutafuta sababu za kumshtaki
Danieli kuhusu usimamizi wake wa shughuli
za serikali, lakini hawakuweza kufanikiwa.
Hawakuweza kupata kosa kwake, kwa sababu
alikuwa mwaminifu, wala hakupatikana na
upotovu au uzembe.
5 Mwishoni watu hawa wakasema, “Kamwe
hatutapata msingi wa mashtaka dhidi ya huyu
Danieli, isipokuwa iwe inahusiana na sheria ya
Mungu wake.”
6 Basi wasimamizi na wakuu wakaingia kwa
mfalme kama kikundi, wakasema, “Ee Mfalme
Dario, uishi milele!
7 Wasimamizi wa ufalme, wasaidizi, wakuu,
washauri na watawala wote wamekubaliana
kwamba mfalme atoe sheria na kukazia amri

kuwa yeyote atakayetoa dua kwa mungu au
mwanadamu katika muda huu wa siku thelathini
zijazo, isipokuwa kwako wewe, ee mfalme,
atupwe ndani ya tundu la simba.
8 Sasa, ee mfalme, toa amri na uiandike ili
isiweze kubadilishwa: kulingana na sheria za
Wamedi na Waajemi, ambazo haziwezi kubatil-
ishwa.”
9 Hivyo Mfalme Dario akaiweka amri hiyo
katika maandishi.
10 Basi Danieli alipofahamu kuwa amri
ile imetangazwa, alienda nyumbani mwake
kwenye chumba chake cha ghorofani, ambako
madirisha yalifunguka kuelekea Yerusalemu.
Akapiga magoti na kuomba mara tatu kwa siku,
akimshukuru Mungu wake, kama alivyokuwa
akifanya awali.
11 Ndipo watu hawa wakaenda kama kikundi
na kumkuta Danieli akiomba na kumsihi Mungu
kwa ajili ya msaada.
12 Basi wakaenda kwa mfalme na kusema
naye kuhusu amri ya mfalme: “Je, hukutangaza
amri kwamba kwa muda huu wa siku the-
lathini zijazo mtu ambaye atamwomba mungu
au mwanadamu yeyote isipokuwa wewe, ee
mfalme, angetupwa ndani ya tundu la simba?”

Mfalme akajibu, “Amri ndivyo ilivyo, kulin-
gana na sheria za Wamedi na Waajemi, ambazo
haziwezi kubatilishwa.”
13 Ndipo wakamwambia mfalme, “Danieli, am-
baye ni mmoja wa mahamisho kutoka Yuda,
hakuheshimu, ee mfalme, wala hajali amri uliy-
oiweka kwa maandishi. Bado anaomba mara
tatu kwa siku.”

14 Mfalme aliposikia hili, akahuzunika mno. Akakusudia kumwokoa Danieli, hivyo akafanya kila jitihada ya kumwokoa hadi jua likatua.
15 Ndipo wale watu wakamwendea mfalme kama kikundi na kumwambia, "Ee mfalme, kumbuka kwamba kulingana na sheria ya Wamedi na Waajemi, hakuna amri wala sheria ambayo mfalme ameitoa inayoweza kubadilishwa."
16 Basi mfalme akatoa amri, nao wakamleta Danieli, wakamtupa ndani ya tundu la simba. Mfalme akamwambia Danieli, "Mungu wako unayemtumikia daima na akuokoe!"
17 Jiwe likaletwa na kuwekwa kwenye mlango wa tundu, naye mfalme akalitia muhuri kwa pete yake mwenyewe pamoja na kwa pete za wakuu wake, ili hali ya Danieli isiweze kubadilishwa.
18 Kisha mfalme akarudi kwenye jumba lake la kifalme, naye usiku kucha hakuweza kula wala kutumia viburudisho alivyoletewa, na hakuweza kulala.
19 Asubuhi na mapema, mfalme akaondoka na kuharakisha kwenda kwenye tundu la simba.
20 Alipokaribia lile tundu, mfalme akamwita Danieli kwa sauti ya uchungu: "Danieli, mtumishi wa Mungu aliye hai! Je, Mungu wako, unayemtumikia daima, ameweza kukuokoa kwa simba?"
21 Danieli akajibu, "Ee mfalme, uishi milele!
22 Mungu wangu alimtuma malaika wake, naye akafunga vinywa vya hawa simba. Hawajanidhuru, kwa sababu nilionekana sina hatia mbele zake. Wala kamwe sijafanya jambo lolote baya mbele yako, ee mfalme."

23 Basi Mfalme akafurahi mno, akatoa amri
Danieli atolewe kutoka kwa lile tundu. Danieli
alipotolewa kutoka kwa lile tundu, hakukutwa
na jeraha lolote, kwa sababu alikuwa amemtu-
maini Mungu wake.
24 Kwa amri ya mfalme, wale watu waliokuwa
wamemshtaki Danieli kwa uongo waliletwa na
kutupwa ndani ya lile tundu la simba, pamoja
na wake zao na watoto wao. Nao kabla hawa-
jafika chini kwenye sakafu ya lile tundu, simba
wakawakamata na kusaga mifupa yao yote.
25 Kisha Mfalme Dario akawaandikia watu wa
makabila yote, na mataifa, na wa kila lugha
duniani kote:

"Mafanikio yawe kwenu sana!

26 "Natoa amri hii, kwamba katika kila
sehemu ya ufalme wangu, lazima watu
wamwogope na kumheshimu Mungu wa
Danieli.

"Kwa maana yeye ni Mungu aliye hai,
naye hudumu milele.
Ufalme wake hautaangamizwa,
nao utawala wake hauna mwisho.
27 Huponya na kuokoa;
hufanya ishara na maajabu
mbinguni na duniani.
Amemwokoa Danieli
kutoka nguvu za simba."

28 Hivyo Danieli akastawi wakati wa utawala
wa Dario, na utawala wa Koreshi Mwajemi.

# 7

*Ndoto ya Danieli ya wanyama wanne*

1 Katika mwaka wa kwanza wa utawala
wa Belshaza mfalme wa Babeli, Danieli
aliota ndoto, nayo maono yakapita mawazoni
mwake alipokuwa amelala kitandani mwake.
Akayaandika mambo aliyoyaona katika ndoto
yake.
2 Danieli akasema: “Katika maono yangu usiku
nilitazama, na hapo mbele yangu kulikuwa na
pepo kutoka pande nne za mbingu, zikivuruga
bahari kuu.
3 Wanyama wanne wakubwa, kila mmoja to-
fauti na mwenzake, wakajitokeza kutoka bahari.
4 “Mnyama wa kwanza alifanana na simba,
naye alikuwa na mabawa ya tai. Nikatazama
hadi mabawa yake yalipong’olewa, naye akain-
uliwa katika nchi, akasimama kwa miguu miwili
kama mwanadamu, naye akapewa moyo wa
binadamu.
5 “Hapo mbele yangu kulikuwa na mnyama
wa pili, aliyefanana na dubu. Upande wake
mmoja alikuwa ameinuka, na alikuwa na mbavu
tatu katika kinywa chake kati ya meno yake.
Akaambiwa, ‘Amka, ule nyama, ushibe!’
6 “Baada ya huyo, nilitazama, na mbele yangu
kulikuwa na mnyama mwingine, aliyefanana na
chui. Juu ya mgongo wake alikuwa na mabawa
manne kama ya ndege. Mnyama huyu alikuwa
na vichwa vinne, naye akapewa mamlaka ya
kutawala.
7 “Baada ya huyo, katika maono yangu usiku
nilitazama, na mbele yangu kulikuwa na
mnyama wa nne, mwenye kutisha na kuogofya,
tena mwenye nguvu nyingi. Alikuwa na

meno makubwa ya chuma; akapondaponda na kuangamiza wahanga wake, na kukanyaga chini ya nyayo zake chochote kilichosalia. Alikuwa tofauti na wanyama wote waliotangulia, naye alikuwa na pembe kumi.

8 “Nilipokuwa nikifikiri kuhusu pembe hizo,
mbele yangu kulikuwa na pembe nyingine,
ndogo, iliyojitokeza miongoni mwa zile kumi;
pembe tatu za mwanzoni ziling’olewa ili kuipa
nafasi hiyo ndogo. Pembe hii ilikuwa na macho
kama ya mwanadamu, na mdomo ulionena kwa
majivuno.

9 “Nilipoendelea kutazama,
“viti vya utawala vikawekwa,
naye Mzee wa Siku akaketi.
Mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji;
nywele za kichwa chake zilikuwa nyeupe kama sufu.
Kiti chake cha enzi kilikuwa kinawaka miali ya moto,
nayo magurudumu yake yote yalikuwa yanawaka moto.
10 Mto wa moto ulikuwa unatiririka,
ukipita mbele yake.
Maelfu elfu wakamhudumia;
kumi elfu mara kumi elfu wakasimama mbele zake.
Mahakama ikakaa kuhukumu,
na vitabu vikafunguliwa.

11 “Kisha nikaendelea kutazama kwa sababu
ya yale maneno ya majivuno yaliyosemwa na
ile pembe. Nikaendelea kuangalia hadi yule
mnyama alipouawa, na mwili wake ukaharibiwa
na kutupwa katika ule moto uliowaka.

12 (Wanyama wengine walikuwa wamevuliwa
mamlaka yao, lakini waliruhusiwa kuishi kwa
muda.)
13 “Katika maono yangu ya usiku nilitazama, na
mbele yangu nikamwona mtu kama Mwana wa
Adamu, akija pamoja na mawingu ya mbinguni.
Akamkaribia huyo Mzee wa Siku, na akaon-
gozwa mbele zake.
14 Akapewa mamlaka, utukufu na ufalme
wenye nguvu; nao watu wa makabila yote,
na mataifa, na wa kila lugha wakamwabudu.
Utawala wake ni utawala wa milele ambao hau-
tapita, nao ufalme wake ni ule ambao kamwe
hautaangamizwa.

### *Tafsiri ya ndoto ya hao wanyama*

15 “Mimi Danieli nilipata mahangaiko rohoni,
nayo maono yale yaliyopita ndani ya mawazo
yangu yalinisumbua.
16 Nikamkaribia mmoja wa wale waliosimama
pale, nikamuuliza maana halisi ya haya yote.

“Basi akaniambia na kunipa tafsiri ya vitu hivi:
17 ‘Hao wanyama wanne wakubwa ni falme
nne zitakazoinuka duniani.
18 Lakini watakatifu wa Yeye Aliye Juu Sana
watapokea ufalme na kuumiliki milele: naam,
milele na milele.’
19 “Kisha nilitaka kufahamu maana ya kweli ya
mnyama yule wa nne, aliyekuwa tofauti na wale
wengine wote, tena wa kutisha sana, na meno
yake ya chuma na makucha ya shaba: mnyama
ambaye alipondaponda na kuangamiza wahanga
wake, na kukanyaga chochote kilichosalia.

20 Pia mimi nilitaka kujua kuhusu zile pembe
kumi juu ya kichwa chake, na pia kuhusu ile
pembe nyingine iliyojitokeza, ambayo mbele
yake zile tatu za mwanzoni zilianguka, ile pembe
ambayo ilionekana kuvutia macho kuliko zile
nyingine, na ambayo ilikuwa na macho na
kinywa kilichonena kwa majivuno.
21 Nilipoendelea kutazama, pembe hii
ilikuwa inapigana vita dhidi ya watakatifu na
kuwashinda,
22 hadi huyo Mzee wa Siku alipokuja na ku-
tamka hukumu kwa kuwapa ushindi watakatifu
wa Yeye Aliye Juu Sana, na wakati ukawadia
walipoumiliki ufalme.
23 "Alinipa maelezo haya: 'Mnyama wa nne
ni ufalme wa nne ambao utatokea duniani.
Utakuwa tofauti na falme nyingine zote, nao
utaharibu dunia nzima, ukiikanyaga chini na
kuipondaponda.
24 Zile pembe kumi ni wafalme kumi watakao-
tokana na ufalme huu. Baada yao mfalme
mwingine atainuka, ambaye atakuwa tofauti na
wale waliotangulia, naye atawaangusha wafalme
watatu.
25 Atanena maneno kinyume cha Yeye Aliye
Juu Sana na kuwatesa watakatifu wake, huku
akijaribu kubadili majira na sheria. Watakatifu
watatiwa chini ya mamlaka yake kwa wakati,
nyakati mbili, na nusu wakati*.
26 " 'Lakini mahakama itakaa kuhukumu, nayo
mamlaka yake yataondolewa na kuangamizwa

* **7:25** au *chini ya mamlaka yake kwa mwaka mmoja, miaka miwili, na nusu mwaka*

kabisa milele.
27 Ndipo ufalme, mamlaka na ukuu wa
falme chini ya mbingu yote zitakabidhiwa kwa
watakatifu, watu wa Yeye Aliye Juu Sana. Ufalme
wake utakuwa ufalme wa milele, nao watawala
wote watamwabudu na kumtii yeye.'
28 "Huu ndio mwisho wa jambo lile. Mimi
Danieli nilitaabika sana katika mawazo yangu,
nao uso wangu ukabadilika, lakini nililiweka
jambo hilo moyoni mwangu."

# 8

## *Maono ya Danieli ya kondoo dume na beberu*

1 Katika mwaka wa tatu wa utawala wa Mfalme
Belshaza, mimi Danieli nilipata maono, baada ya
maono yaliyokuwa yamenitokea awali.
2 Katika maono yangu, nilijiona nikiwa ndani
ya ngome ya Shushani katika jimbo la Elamu;
katika maono nilikuwa kando ya Mto Ulai*.
3 Nikatazama juu, na hapo mbele yangu ku-
likuwa na kondoo dume mwenye pembe mbili,
akiwa amesimama kando ya mto, nazo pembe
zake zilikuwa ndefu. Pembe moja ilikuwa ndefu
kuliko hiyo nyingine, lakini iliendelea kukua
baadaye.
4 Nikamtazama yule kondoo dume alivyokuwa
akishambulia kuelekea magharibi, kaskazini na
kusini. Hakuna mnyama yeyote aliyeweza
kusimama mbele yake, wala hakuna aliyeweza
kuokoa kutoka nguvu zake. Akafanya kama
alivyopenda, naye akawa mkuu.

* **8:2** huu ni mfereji uliopitia kati ya Shushani

5 Nilipokuwa ninatafakari hili, ghafula beberu mwenye pembe moja kubwa katikati ya macho yake alikuja kutoka magharibi, akiruka kasi juu ya dunia yote bila kugusa ardhi.
6 Alikuja akimwelekea yule kondoo dume mwenye pembe mbili niliyemwona akisimama kando ya mto, akamshambulia kwa hasira nyingi.
7 Nikamwona akimshambulia yule kondoo dume kwa hasira nyingi, akampiga yule kondoo dume na kuvunja pembe zake mbili. Yule kondoo dume hakuwa na nguvu za kumzuia yule beberu; huyo beberu akamwangusha yule kondoo dume chini na kumkanyaga, wala hakuna aliyeweza kumwokoa yule kondoo dume kutoka nguvu za huyo beberu.
8 Yule beberu akawa mkubwa sana, lakini katika kilele cha nguvu zake, ile pembe yake ndefu ilivunjika, na mahali pake pakaota pembe nne kubwa kuelekea pande nne za dunia.
9 Kutoka mojawapo ya zile pembe nne palitokea pembe ndogo, nayo ikaongezeka nguvu kuelekea kusini, na mashariki, na Nchi ya Kupendeza.
10 Pembe hiyo ikaendelea kukua hadi kufikia jeshi la mbinguni, nayo ikalitupa baadhi ya nyota za jeshi la angani chini duniani, na kuzikanyaga.
11 Pembe hiyo ikajikweza ili iwe kama Mkuu wa hilo jeshi la Mwenyezi Mungu; ikamwondolea Mwenyezi Mungu dhabihu ya kila siku, napo mahali pake patakatifu pakashushwa chini.
12 Kwa sababu ya uasi, jeshi la watakatifu na dhabihu za kila siku vikatiwa mkononi mwake.

Pembe hiyo ikafanikiwa katika kila kitu ili-
chofanya, nayo kweli ikatupwa chini.

13 Kisha nikamsikia mtakatifu mmoja
akizungumza na mtakatifu mwingine,
akamwambia, “Je, itachukua muda gani maono
haya yatimie: maono kuhusu dhabihu ya kila
siku, uasi unaosababisha ukiwa, kutwaliwa kwa
mahali patakatifu, na jeshi litakalokanyagwa
chini ya nyayo?”

14 Akaniambia, “Itachukua jioni na asubuhi
elfu mbili na mia tatu; ndipo mahali patakatifu
patawekwa wakfu tena.”

*Tafsiri ya maono hayo*

15 Mimi Danieli nilipokuwa ninaangalia maono
na kujaribu kuelewa, mbele yangu alisimama
mmoja aliyefanana na mwanadamu.

16 Kisha nikasikia sauti ya mwanadamu kutoka
Mto Ulai ikiita, “Jibraili, mwambie mtu huyu
maana ya maono haya.”

17 Alipokuwa akikaribia pale nilipokuwa
nimesimama, niliogopa, nikaanguka kifudifudi.
Akaniambia, “Mwana wa mwanadamu, fahamu
kuwa maono haya yanahusu siku za mwisho.”

18 Alipokuwa akinena nami, nilikuwa katika
usingizi mzito, huku nimelala kifudifudi. Ndipo
aliponigusa na kunisimamisha wima.

19 Akaniambia, “Nitakuambia yale
yatakayotokea baadaye wakati wa ghadhabu,
kwa sababu maono haya yanahusu wakati wa
mwisho ulioamriwa.

20 Kondoo dume mwenye pembe mbili ambaye ulimwona anawakilisha wafalme wa Umedi na Uajemi.
21 Yule beberu mwenye manyoya mengi ni mfalme wa Uyunani, nayo ile pembe ndefu katikati ya macho yake ni mfalme wa kwanza.
22 Zile pembe nne zilizoota badala ya ile pembe iliyovunjika zinawakilisha falme nne ambazo zitatokea kutoka taifa lake, lakini hakuna hata mmoja utakaokuwa na nguvu kama ile pembe iliyovunjika.

23 "Katika sehemu ya mwisho ya utawala wao, waasi watakapokuwa waovu kabisa, atainuka mfalme mwenye uso mkali, aliye stadi wa hila.
24 Atakuwa na nguvu nyingi, lakini si kwa uwezo wake mwenyewe. Atasababisha uharibifu wa kutisha, na atafanikiwa kwa chochote anachofanya. Atawaangamiza watu maarufu na watu watakatifu.
25 Atasababisha udanganyifu ustawi, naye atajihesabu mwenyewe kuwa bora kuliko wote. Wakati watajisikia kuwa salama, atawaangamiza wengi, na kushindana na Mkuu wa wakuu. Lakini ataangamizwa, isipokuwa si kwa uwezo wa mwanadamu.

26 "Maono kuhusu jioni na asubuhi ambayo umepewa ni kweli, lakini yatie muhuri maono haya, kwa maana yanahusu nyakati za baadaye sana."

27 Mimi Danieli nilikuwa nimechoka sana, na nikalala nikiwa mgonjwa kwa siku kadhaa. Ndipo nikaamka, nikaendelea na shughuli

za mfalme. Nilifadhaishwa na maono hayo; sikuweza kuyaelewa.

# 9

*Maombi ya Danieli*

1 Katika mwaka wa kwanza wa utawala wa
Dario mwana wa Ahasuero (mzaliwa wa Umedi),
ambaye alifanywa mtawala wa ufalme wa Babeli,
2 katika mwaka wa kwanza wa utawala
wake, mimi Danieli nilielewa kutokana na
Maandiko, kulingana na neno la Mwenyezi
Mungu lililopewa nabii Yeremia, kwamba ukiwa
wa Yerusalemu ungetimizwa kwa miaka sabini.
3 Kwa hiyo nikamgeukia Mwenyezi Mungu na
kumsihi katika maombi na dua, katika kufunga,
na kuvaa gunia na kujipaka majivu.

4 Nikamwomba Mwenyezi Mungu, Mungu
wangu, na kutubu:

“Ee Bwana, Mungu mkuu na unayetisha, anayeshika agano lake la upendo kwao wanaompenda na kutii maagizo yake,

5 tumetenda dhambi na kufanya mabaya.
Tumekuwa waovu na tumeasi; tumegeuka mbali
na maagizo yako na sheria zako.
6 Hatukuwasikiliza watumishi wako man-
abii, ambao kwa jina lako walisema na wafalme
wetu, wakuu wetu, baba zetu, na watu wote wa
nchi.
7 “Bwana, wewe ni mwenye haki, lakini siku
hii ya leo tumefunikwa na aibu: watu wa Yuda,
na wakaaji wa Yerusalemu, na Waisraeli wote,
walio karibu na walio mbali, katika nchi zote

ulikotutawanya kwa sababu tulikosa uaminifu kwako.

8 Ee Mwenyezi Mungu, sisi na wafalme wetu,
wakuu wetu na baba zetu tumefunikwa na aibu
kwa sababu tumefanya dhambi dhidi yako.

9 Bwana Mungu wetu ni mwenye rehema na
anayesamehe, hata ingawa tumefanya uasi dhidi
yake.

10 Hatukumtii Mwenyezi Mungu, Mungu
wetu, wala kuzishika sheria alizotupatia kupitia
kwa watumishi wake, manabii.

11 Israeli wote wamekosea sheria yako na
kugeuka mbali, nao wamekataa kukutii.

“Kwa hiyo laana na viapo vya hukumu vilivyoandikwa katika Torati ya Musa, mtumishi wa Mungu, vimemiminwa juu yetu, kwa sababu tumefanya dhambi dhidi yako.

12 Umetimiza maneno uliyosema dhidi yetu
na dhidi ya watawala wetu, kwa kuleta maafa
makubwa juu yetu. Chini ya mbingu yote kamwe
hapajatendeka kitu kama kile kilichotendeka
kwa Yerusalemu.

13 Kama vile ilivyoandikwa katika Torati ya
Musa, misiba hii yote imekuja juu yetu, lakini
hatujaomba fadhili za Mwenyezi Mungu, Mungu
wetu, kwa kuacha kutenda dhambi na kuisikiliza
kweli yake.

14 Mwenyezi Mungu hakusita kuleta maafa
juu yetu, kwa maana Mwenyezi Mungu, Mungu
wetu, ni mwenye haki katika kila afanyalo; lakini
hata hivyo, hatujamtii.

15 “Sasa, Ee Bwana Mungu wetu, uliyewatoa
watu wako Misri kwa mkono wenye nguvu, na

kujifanyia Jina linalodumu hadi leo, tumetenda dhambi, tumefanya mabaya.

16 Ee Bwana, kwa kadiri ya matendo yako
ya haki, ondoa hasira yako na ghadhabu yako kwa Yerusalemu, mji wako, mlima wako mtakatifu. Dhambi zetu na maovu ya baba zetu yameifanya Yerusalemu na watu wako kitu cha kudharauliwa kwa wale wote wanaotuzunguka.

17 "Basi Mungu wetu, sasa sikia maombi na
dua za mtumishi wako. Ee Bwana, kwa ajili yako angalia kwa huruma ukiwa wa mahali pako patakatifu.

18 Ee Mungu, tega sikio, ukasikie; fumbua
macho yako ukaone ukiwa wa mji ule wenye Jina lako. Hatukutolei maombi yetu kwa sababu sisi tuna haki, bali kwa sababu ya rehema zako nyingi.

19 Ee Bwana, sikiliza! Ee Bwana, samehe! Ee
Bwana, sikia na ukatende! Kwa ajili yako, Ee Mungu wangu, usikawie, kwa sababu mji wako na watu wako wanaitwa kwa Jina lako."

### *Majuma sabini*

20 Basi, nilipokuwa bado nikinena na kuomba,
nikiungama dhambi yangu na dhambi ya watu wangu Israeli, na nikifanya maombi yangu kwa Mwenyezi Mungu, Mungu wangu, kwa ajili ya mlima wake mtakatifu,

21 wakati nilipokuwa bado katika maombi, Ji-
braili, yule mtu niliyekuwa nimemwona katika maono hapo awali, alinijia kwa kasi karibu wakati wa kutoa dhabihu ya jioni.

22 Akanielimisha na kuniambia, “Danieli, sasa
nimekuja kukupa akili na ufahamu.
23 Mara ulipoanza kuomba, jibu lilitolewa, am-
balo nimekuja kukupasha habari, kwa maana
wewe unapendwa sana. Kwa hiyo, tafakari
ujumbe huu na uelewe maono haya:

24 “Majuma sabini yameamriwa kwa ajili ya
watu wako na kwa ajili ya mji wako mtakatifu, ili
kumaliza makosa, kukomesha dhambi, kufanya
upatanisho kwa ajili ya uovu, kuleta haki ya
milele, kutia muhuri maono na unabii, na pia
kumpaka mafuta yeye aliye mtakatifu sana.

25 “Ujue na kuelewa hili: Tangu kutolewa
kwa amri ya kuutengeneza na kuujenga upya
Yerusalemu hadi kuja kwa Mpakwa mafuta, aliye
mtawala, kutakuwa na majuma saba, na ma-
juma sitini na mawili. Barabara zitajengwa tena
pamoja na mahandaki, lakini katika wakati wa
taabu.
26 Baada ya majuma sitini na mawili, Mpakwa
Mafuta atakatiliwa mbali, wala hatabaki na kitu.
Watu wa mtawala atakayekuja watauharibu mji
pamoja na mahali patakatifu. Mwisho utakuja
kama mafuriko: Vita vitaendelea hadi mwisho,
nao ukiwa umeamriwa.
27 Mtawala huyo atathibitisha agano na watu
wengi kwa juma moja. Katikati ya juma
hilo atakomesha dhabihu na sadaka. Ma-
hali pa dhabihu katika Hekalu, atasimamisha
chukizo la uharibifu, hadi mwisho ulioamriwa
utakapomiminwa juu yake yeye aletaye uharib-
ifu.”

# 10

## *Maono ya Danieli kuhusu mtu*

1 Katika mwaka wa tatu wa utawala wa Koreshi
mfalme wa Uajemi, Danieli (ambaye aliitwa Bel-
teshaza) alipewa ufunuo. Ujumbe wake ulikuwa
kweli, nao ulihusu vita vikubwa. Ufahamu wa
ujumbe ulimjia katika maono.
2 Wakati huo, mimi Danieli nikaomboleza kwa
majuma matatu.
3 Sikula chakula kizuri; nyama wala divai
havikugusa midomo yangu; nami sikujipaka
mafuta kamwe hadi majuma matatu yalipotimia.
4 Siku ya ishirini na nne ya mwezi wa kwanza,
nilikuwa nimesimama kwenye ukingo wa mto
mkubwa Hidekeli*.
5 Nikatazama juu, na mbele yangu palikuwa
na mtu aliyevaa mavazi ya kitani na mshipi wa
dhahabu safi kutoka Ufazi kiunoni mwake.
6 Mwili wake ulikuwa kama zabarajadi safi,
uso wake kama radi, macho yake kama miali wa
moto, mikono yake na miguu yake kama mng'ao
wa shaba iliyosuguliwa, nayo sauti yake kama ya
umati mkubwa wa watu.
7 Ni mimi Danieli peke yangu niliyeona
hayo maono; watu waliokuwa pamoja nami
hawakuyaona, lakini waligubikwa na hofu kuu,
hata wakakimbia na kujificha.
8 Kwa hiyo niliachwa peke yangu, nikitazama
maono hayo makubwa; sikubakiwa na nguvu, na
rangi ya uso wangu ikabadilika kama aliyekufa,
nikakosa nguvu.

---

* **10:4** yaani *Mto Tigrisi*

9 Kisha nikamsikia akisema, nami nilipokuwa
nikimsikiliza, nikapatwa na usingizi mzito,
nikalala kifudifudi.
10 Mkono ulinigusa, ukaninyanyua na kuni-
weka magotini, mikono yangu ikishika chini,
huku nikiwa bado ninatetemeka.
11 Akasema, “Danieli, wewe mtu upendwaye
sana, fikiri kwa makini maneno ninayoenda
kunena nawe; simama wima, kwa maana sasa
nimetumwa kwako.” Aliponiambia haya, nikasi-
mama nikitetemeka.
12 Ndipo akaendelea kusema, “Danieli, usio-
gope. Tangu siku ya kwanza ulipotia moyo
wako kupata ufahamu na kujinyenyekeza mbele
ya Mungu wako, maneno yako yalisikiwa, nami
nimekuja kwa ajili ya maneno yako.
13 Lakini mkuu wa ufalme wa Uajemi alin-
ipinga kwa siku ishirini na moja. Ndipo Mikaeli,
mmoja wa malaika wakuu, alikuja kunisaidia,
kwa sababu nilikuwa nimezuiliwa huko na
mfalme wa Uajemi.
14 Sasa nimekuja kukuelezea mambo yatakay-
owatokea watu wako wakati ujao, kwa maana
maono hayo yanahusu wakati ambao haujaja
bado.”
15 Alipokuwa akiniambia haya, nilisujudu, uso
wangu ukigusa chini, nikawa bubu.
16 Ndipo mmoja aliyeonekana kama
mwanadamu akanigusa midomo yangu, nami
nikafungua kinywa changu, nikaanza kunena.
Nikamwambia yule aliyesimama mbele yangu,
“Nimepatwa na huzuni kubwa kwa sababu ya
maono haya, bwana wangu, nami nimeishiwa
nguvu.

17 Bwana wangu, mimi mtumishi wako nitawezaje kuzungumza na wewe? Nguvu zangu zimeniishia, hata ninashindwa kupumua."

18 Tena yule aliyeonekana kama mwanadamu akanigusa na kunitia nguvu.
19 Akasema, "Ee mtu upendwaye sana, usiogope. Amani iwe kwako! Uwe na nguvu sasa; jipe nguvu."

Alipozungumza nami, nilipata nguvu, nikasema, "Nena, bwana wangu, kwa kuwa umenipa nguvu."

20 Kwa hiyo akasema, "Je, unajua kwa nini nimekujia? Sasa hivi nitarudi kupigana dhidi ya mkuu wa Uajemi, nami nikienda, mkuu wa Uyunani atakuja.
21 Lakini kwanza nitakuambia kile kilichoandikwa katika Kitabu cha Kweli. (Hakuna hata mmoja anayenisaidia dhidi yao isipokuwa Mikaeli, mkuu wenu.

# 11

1 Nami katika mwaka wa kwanza wa utawala wa Dario Mmedi, nilisimama kumsaidia na kumlinda.)

## *Wafalme wa kusini na kaskazini*

2 "Sasa basi, ninakuambia kweli: Wafalme wengine watatu watatokea Uajemi. Kisha atatokea mfalme wa nne, ambaye atakuwa tajiri sana kuliko wengine wote. Atakapokuwa amekwisha kujipatia nguvu kwa utajiri wake, atamchochea kila mmoja dhidi ya ufalme wa Uyunani.

3 Ndipo mfalme mwenye nguvu atatokea, atakayetawala kwa nguvu nyingi, na kufanya anavyopenda.
4 Baada ya kujitokeza, himaya yake itavunjwa na kugawanyika katika pande nne za mbinguni. Hautaenda kwa wazao wake, wala hautakuwa na nguvu alizokuwa nazo, kwa sababu himaya yake itang'olewa na kupewa wengine.

5 “Mfalme wa Kusini atakuwa na nguvu, lakini mmoja wa majemadari wake atakuwa na nguvu zaidi yake, naye atatawala ufalme wake mwenyewe kwa nguvu nyingi.
6 Baada ya miaka kadhaa, wataungana. Binti ya mfalme wa Kusini ataolewa kwa mfalme wa Kaskazini ili kuimarisha mapatano, lakini nguvu za huyo binti hazitadumu; hata mfalme hatadumu wala nguvu zake. Katika siku hizo atafukuzwa, pamoja na hao wasindikizaji wake wa kifalme, na baba yake, na yeyote aliyemuunga mkono.
7 “Mmoja kutoka jamaa ya huyo binti atainuka na kuchukua nafasi yake. Atashambulia majeshi ya mfalme wa Kaskazini na kuingia katika ngome yake; atapigana dhidi yao, naye atashinda.
8 Tena ataitwaa miungu yao, vinyago vyao vya chuma, na vitu vyao vya thamani vya fedha na dhahabu, na kuvichukua hadi Misri. Kwa miaka kadhaa atamwacha mfalme wa Kaskazini bila kumsumbua.
9 Kisha mfalme wa Kaskazini atashambulia nchi ya mfalme wa Kusini, lakini atarudi hadi kwenye nchi yake mwenyewe.
10 Wana wa mfalme wa Kaskazini watajiandaa

kwa vita na kukusanya jeshi kubwa, ambalo
litafagia nchi kama mafuriko yasiyozuilika, na
kuendelea na vita hadi kwenye ngome ya mfalme
wa Kusini.
11 “Kisha mfalme wa Kusini atatoka kwa
ghadhabu na kupigana dhidi ya mfalme wa
Kaskazini, ambaye atakusanya jeshi kubwa,
lakini litashindwa.
12 Jeshi litakapotekwa, mfalme wa Kusini ata-
jawa na kiburi, na atachinja maelfu mengi; hata
hivyo hatabaki na ushindi.
13 Kwa maana mfalme wa Kaskazini ataku-
sanya jeshi kubwa kuliko lile la kwanza; baada
ya miaka kadhaa, atasonga mbele na jeshi kubwa
mno lililoandaliwa vizuri.
14 “Katika nyakati hizo, wengi watainuka dhidi
ya mfalme wa Kusini. Watu wenye ghasia
miongoni mwa watu wako mwenyewe wataasi ili
kutimiza maono, lakini bila mafanikio.
15 Ndipo mfalme wa Kaskazini atakuja na ku-
uzingira mji kwa majeshi, na kuuteka mji wa
ngome. Majeshi ya Kusini yatakosa nguvu za
kumzuia; naam, hata vikosi vyao vya askari
vilivyo bora zaidi, havitakuwa na nguvu za
kuwakabili.
16 Huyo mvamia nchi atafanya apendavyo;
hakuna yeyote atakayeweza kumpinga. Ataji-
imarisha katika Nchi ya Kupendeza, na atakuwa
na uwezo wa kuiangamiza.
17 Ataamua kuja na nguvu za ufalme wake
wote, na kufanya mapatano ya amani na mfalme
wa Kusini. Naye atamtoa binti yake aolewe
naye ili kuuangusha ufalme, lakini mipango yake
haitafanikiwa wala kumsaidia.

18 Ndipo atabadili nia yake na kupigana na nchi za pwani na aziteke nyingi, lakini jemadari mmoja atakomesha ufidhuli wake, na kurudisha ufidhuli wake juu yake.

19 Baada ya hili atazigeukia ngome za nchi yake mwenyewe, lakini atajikwaa na kuanguka, wala hataonekana tena.

20 "Atakayetawala baada yake atamtuma mtoza ushuru ili kudumisha fahari ya kifalme. Hata hivyo, baada ya miaka michache ataangamizwa, lakini si katika hasira wala katika vita.

21 "Atakayetawala baada yake atakuwa mtu wa kudharauliwa ambaye hajapewa heshima ya kifalme. Atauvamia ufalme wakati watu wake wanapojiona kuwa salama, naye atautwaa kwa hila.

22 Ndipo jeshi kubwa litafagiliwa mbele yake; jeshi pamoja na mkuu mmoja wa agano wataangamizwa.

23 Baada ya kufanya mapatano naye, atatenda kwa udanganyifu, na ataingia madarakani akitumia watu wachache tu.

24 Wakati majimbo yaliyo tajiri sana yanajiona salama, atayavamia, naye atatimiza kile baba zake na babu zake hawakuweza. Atagawa nyara, mateka na utajiri miongoni mwa wafuasi wake. Atapanga njama ya kupindua miji yenye ngome, lakini kwa muda mfupi tu.

25 "Atachochea nguvu zake na ushujaa wake kwa jeshi kubwa dhidi ya mfalme wa Kusini. Mfalme wa Kusini atafanya vita na jeshi kubwa lenye nguvu sana, lakini hataweza kusimama kwa sababu ya hila zilizopangwa dhidi yake.

26 Wale wanaokula kutoka meza ya mfalme
watajaribu kumwangamiza; jeshi lake litafag-
iliwa mbali, nao wengi watakufa vitani.
27 Wafalme hawa wawili, mioyo yao ikiwa
imekusudia mabaya, wataketi kwenye meza
moja na kudanganyana wao kwa wao, lakini
pasipo faida, kwa sababu bado mwisho utakuja
katika wakati ulioamriwa.
28 Mfalme wa Kaskazini atarudi katika nchi
yake na utajiri mwingi, lakini atakuwa ameukaza
moyo wake kinyume cha agano takatifu. At-
achukua hatua dhidi ya hilo agano, kisha arudi
nchi yake.

29 "Wakati ulioamriwa, atavamia tena Kusini,
lakini wakati huu matokeo yake yatakuwa tofauti
na yale ya wakati wa kwanza.
30 Meli za nchi ya Kitimu zitampinga, naye
atavunjika moyo. Ndipo atarudi nyuma na kutoa
hasira yake dhidi ya agano takatifu. Atarudi na
kuonesha fadhili kwa wale wanaoliacha agano
takatifu.
31 "Majeshi yake yenye silaha yatainuka ili
kunajisi ngome ya Hekalu, na kuondolea mbali
sadaka ya kuteketezwa ya kila siku. Ndipo watal-
isimamisha chukizo la uharibifu linalosababisha
ukiwa.
32 Kwa udanganyifu, atapotosha wale walion-
ajisi agano, lakini watu wanaomjua Mungu wao
watampinga kwa uthabiti.

33 "Wenye hekima watawafundisha wengi, in-
gawa kwa kitambo watauawa kwa upanga au
kuchomwa moto, au kukamatwa, au kutekwa
nyara.

34 Watakapoanguka, watapokea msaada ki-
dogo, nao wengi wasio waaminifu wataungana
nao.
35 Baadhi ya wenye hekima watajikwaa, ili
waweze kusafishwa, kutakaswa na kufanywa
wasio na waa hadi wakati wa mwisho, kwa
maana bado litakuja kwa wakati ulioamriwa.

### *Mfalme ajikwezaye mwenyewe*

36 “Mfalme atafanya apendavyo. Atajikweza
na kujitukuza juu ya kila mungu, naye atasema
mambo ambayo hayajawahi kusikiwa dhidi ya
Mungu wa miungu. Atafanikiwa hadi wakati
wa ghadhabu utimie, kwa maana kile kili-
chokusudiwa lazima kitatukia.
37 Hataonesha heshima kwa miungu ya baba
zake au kwa yule aliyetamaniwa na wanawake,
wala hatajali mungu yeyote, bali atajikweza
mwenyewe juu yao wote.
38 Badala ya kuwajali miungu, ataheshimu
mungu wa ngome; mungu ambaye hakujulikana
na baba zake ndiye atamheshimu kwa dhahabu
na fedha, kwa vito vya thamani, na zawadi za
thamani kubwa.
39 Atashambulia ngome zenye nguvu mno
kwa msaada wa mungu wa kigeni, naye
atawaheshimu sana wale watakaomkubali
yeye. Atawafanya watawala wa watu wengi,
na atagawa nchi kwa gharama.

40 “Wakati wa mwisho, mfalme wa Kusini at-
apigana naye vita, naye mfalme wa Kaskazini
atamshambulia kwa magari ya vita, askari wa-
panda farasi, na idadi kubwa ya meli. Atavamia

nchi nyingi na kuzikumba nchi hizo kama mafu-
riko.
41 Pia ataivamia Nchi ya Kupendeza. Nchi
nyingi zitapinduliwa, bali Edomu, Moabu, na
viongozi wa Amoni wataokolewa kutoka mkono
wake.
42 Atapanua mamlaka yake juu ya nchi nyingi;
hata Misri haitaepuka.
43 Atamiliki hazina za dhahabu na fedha na
utajiri wote wa Misri, huku Walibia na Wakushi
wakijisalimisha kwake.
44 Lakini taarifa kutoka mashariki na kaskazini
zitamshtua, naye ataondoka kwa ghadhabu
nyingi ili kuangamiza na kuharibu wengi kabisa.
45 Atasimika mahema yake ya ufalme kati ya
bahari na mlima mtakatifu wa kupendeza. Hata
hivyo, atafikia mwisho wake, wala hakuna yey-
ote atakayemsaidia.

# 12

### *Nyakati za mwisho*

1 “Katika wakati huo Mikaeli, mtawala mkuu
ambaye huwalinda watu wako, atainuka. Ku-
takuwako wakati wa taabu ambao haujatokea
tangu mwanzo wa mataifa hadi wakati huo.
Lakini wakati huo, watu wako, kila mmoja am-
baye jina lake litakutwa limeandikwa kwenye
kitabu, ataokolewa.
2 Wengi ambao wamelala kwenye mavumbi
wataamka, baadhi yao kwa uzima wa milele,
wengine kwa aibu na kudharauliwa milele.
3 Wale wenye hekima watang’aa kama mwanga
wa mbingu, nao wale ambao huwaongoza wengi

kutenda haki, watang'aa kama nyota milele na
milele.
4 Lakini wewe Danieli, yafunge na kuyatia
muhuri maneno ya kitabu hiki hadi wakati wa
mwisho. Wengi wataenda hapa na pale, na
maarifa yataongezeka."

5 Ndipo mimi Danieli nikaangalia, nako mbele
yangu walisimama wengine wawili, mmoja
katika ukingo huu wa mto, na mwingine ukingo
wa pili wa mto.
6 Mmoja wao akamwambia yule mtu aliyevaa
nguo za kitani, aliyekuwa juu ya maji ya mto,
"Je, itachukua muda gani kabla mambo haya ya
kushangaza hayajatimizwa?"
7 Kisha mtu yule aliyevaa nguo za kitani,
aliyekuwa juu ya maji ya mto, akainua mkono
wake wa kuume na mkono wake wa kushoto
kuelekea mbinguni, nami nikamsikia akiapa kwa
jina lake yeye aishiye milele, akisema, "Itakuwa
wakati, nyakati mbili, na nusu wakati*. Nguvu
za watu watakatifu zitakapokuwa zimevun-
jwa kabisa, ndipo mambo haya yote yatakapo-
timizwa."
8 Nilisikia, lakini sikuelewa. Kwa hiyo
nikauliza, "Bwana wangu, matokeo ya haya yote
yatakuwa nini?"
9 Akajibu, "Danieli, nenda zako, kwa sababu
maneno haya yamefungwa na kutiwa muhuri
hadi wakati wa mwisho.

---

* **12:7** Wakati, nyakati mbili na nusu wakati maana yake mwaka mmoja, miaka miwili, na nusu mwaka, yaani miaka mitatu na nusu.

10 Wengi watatakaswa, na kuondolewa mawaa
na kufanywa safi, lakini waovu wataendelea
kuwa waovu. Hakuna mmoja wa waovu
atakayefahamu, lakini wale wenye hekima
watafahamu.
11 “Tangu wakati ule wa kukomeshwa kwa
dhabihu ya kila siku, na kuanzishwa kwa chukizo
la uharibifu, kutakuwepo siku elfu moja na mia
mbili na tisini (1,290).
12 Kubarikiwa ni yule atakayevumilia hadi ku-
fikia mwisho wa hizo siku elfu moja mia tatu na
thelathini na tano (1,335).
13 “Lakini wewe, nenda zako hadi mwisho. Uta-
pumzika, nawe mwisho wa hizo siku utafufuka
ili kuupokea urithi uliowekewa.”

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu
## The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

**Creative Commons License**

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: "Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible."

Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: "The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible."

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 20 May 2025 from source files dated 21 May 2025

72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d